
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**Taarifa ya ALMA - Robo ya Kwanza, 2024**

MUUNGANO WA VIONGOZI WA AFRIKA KATIKA UDHIBITI WA MALARIA

# KADI YA ALAMA YA UFUATILIAJI NA UWAJIBIKAJI WA MALARIA




**Vipimo**

| | | |
|---|---|---|
| **Kugharamia** | | |
| Makisio ya fedha za ununuzi wa Vyandarua na Viuatilifu Ukoko kwa kipindi cha (2024-2026) (% ya mahitaji) | | 97 |
| Sekta ya Umma kugharamia Dawa Mseto na Vitendanishi kwa kipindi cha (2024-2026)(% ya mahitaji) | | 100 |
| % ya fedha zilizotengwa kutekeleza Mpango Mkakati wa Malaria kwa kipindi (2024-2026) | | 80 |
| **Sera** | | |
| Kusaini, Kuidhinisha na kuwasilisha Mkataba wa AMA AUC | ▲ | |
| Uwepo wa Mikakati inayolega kambi za wakimbizi kwenye mpango mkakati wa malaria | | |
| Uwepo Uwepo wa Mikakati inayolega watu wa ndani ya nchi wasio na makazi maalum kwenye mpango mkakati wa malaria | | |
| Nchi inatoa taarifa za uzinduzi wa Kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na mimi | | |
| Nchi inatoa taarifa za uzinduzi wa Kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na mimi | | |
| **Ufuatiliaji wa Usugu, Utekelezaji na Matokeo yake** | | |
| Tafiti za kufuatilia ufanisi wa dawa za kutibu malaria umefanyika tangu mwaka 2019 na taarifa zake kutumwa Shirika la Afya Duniani | | |
| Aina ya makundi yaliyothibitishwa kujenga kukabiliwa na usugu dhidi ya mbu kwenye vituo maalum vya ufuatiliaje (Sentinel Sites) | | |
| Ufuatiliaji wa usugu wa mbu dhidi ya viuatilifu tangu 2015 na taarifa kuripotiwa kwa Shirika la Afya Duniani | | |
| Akiba ya vitendanishi (RDTs) (Ya zaidi ya miezi 6) | | |
| Akiba ya dawa mseto (ACTs) (Ya zaidi ya miezi 6) | | |
| Kampeni ya vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu/unyunyuziaji wa dawa ya ukoko (LLINS/IRS) inaenda kwa mujibu na malengo | | |
| Kampeni ya vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu/unyunyuziaji wa dawa ya ukoko (LLINS/IRS) inaenda kwa mujibu na malengo | | 85 |
| Kupungua kwa Idadi ya Visa vipya kwa asilimia 55 au zaidi kwa mwaka 2022 (ukilinganisha na takwimu za 2015) | | |
| Kupungua kwa Idadi ya vifo kwa asilimia 55 au zaidi kwa mwaka 2022 (ukilinganisha na takwimu za mwaka 2015) | | |
| **Viashiria vya Afya ya uzazi, afya ya mtoto na UVIKO 19** | | |
| Idadi waliofikiwa na umezezeshaji wa dawa za kinga tiba dhidi Magonjwa ya Tropiki yaliyosahaulika kwenye jamii (NTD index, %)(2022) | | |
| % ya ugawaji dawa kwa walengwa ili kufikia Malengo ya Shirika la Afya Duniani | | 75 |
| Makadirio ya asilimia ya watoto, kati ya miaka 0-14, waishio na VVU ambao wanapata dawa za ARV (2022) | | 73 |
| Kiwango cha Utoaji wa dozi mbili za vitamin A katika 2022 | | 90 |
| Kiwango cha chanjo ya DPT3 2022 (miongoni mwa watoto wenye miezi 0-11) | | 88 |

Malaria inaathiri karibu maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kukiwa na ongezeko kutegemeana na misimu. Idadi ya wagonjwa wa malaria kwa mwaka 2022 ilikuwa 3,666,741 na vifo 1,538 vilivyotokana na malaria.

**UFUNGUO:**

- Lengo limefikiwa /utekelezaji unaenda sawa
- Juhudi zaidi zinahitajika
- Utekelerzaji upo nje ya lengo
- Hamna Takwimu
- Haihusiki

## Malaria:

Bara la Afrika liko katikati ya dhoruba kubwa linalotokana na tishio la kuvuruga utoaji huduma ambalo linaweza kuathiri maendeleo yaliyopatikana katika udhibiti wa malaria kwa karne zilizopita. Hivyo ni lazima kuchukua hatua za haraka ili kuzuia na kupunguza athari, kufuatia mgogoro wa kifedha duniani, kuongezeka kwa tishio la kibailojia, mabadiliko ya hali ya hewa na madhara ya kibinadamu. Matukio haya yanatishia sana kuvuruga mafanikio yaliyopatikana katika udhibiti wa malaria kwa takriban miaka 20, na huenda yakasababisha ongezeko la majanga na milipuko ya magonjwa, iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa mapema.

Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, zinakabiliwa na pengo la takriban dola za marekani bilioni 1.5 ili kuendeleza huduma zilizopo, ingawa kiasi hicho bado hakitoshelezi mahitaji halisi kwa kipindi hadi kufika mwaka 2026. Ili kuwa na mwenendo sahihi kuelekea kutokomeza malaria, tunahitaji kuhamasisha ili kukusanya fedha zaidi takriban dola za marekani bilioni 5.2 kila mwaka, ili kukidhi mahitaji ya Mpango Mkakati wa Kudhibiti Malaria.

Mabadiliko ya hali ya hewa ni moja ya tishio kubwa la kuharibu mafanikio yaliyopatikana hadi sasa. Bara la Afrika linakabiliwa na hatari inayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa, na ifikapo mwaka 2030, zaidi ya watu milioni 150 watakuwa katika hatari ya kupata maambukizi ya malaria kutokana na ongezeko la joto na wingi wa mvua. Maafa yanayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa, yamefanya mamilioni ya watu kulazimika kuhama makazi yao, kuharibu miundo mbinu ya barabara, na kusababisha changamoto ya watu kushindwa kufika vituoni kupata huduma.

Kunahitajika kupunguza wingi wa ukaa na kiwango cha kaboni. Ili kufanikisha hili, inasisitizwa kutekeleza afua za udhibiti wa malaria kwa uwiano na kushirikisha sekta zingine ili kupata majawabu sahihi kwa changamoto zilizopo. Tunahitaji kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za afya, ili kukabiliana na tishio na madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa na milipuko ya magonjwa. Ni lazima pia kuchukua hatua madhubuti za kukabiliana na usugu wa viuatilifu na dawa za kutibu malaria, kupungua kwa ufanisi wa vipimo vya uchunguzi vinavyotoa majibu kwa haraka, na uwepo wa mbu aina ya *Anofelesi Stephensi* ambae anaeneza malaria katika maeneo yote hasa ya mjini. Habari njema ni kuwa juhudi za kuboresha na kuongeza seti ya zana mbalimbali za kudhibiti malaria zinaendelea kupanuka.

Shirika la Afya Duniani limeidhinisha matumizi ya vyandarua venye viuatilifu makundi mawili kwa pamoja, ambavyo vina ufanisi mkubwa kwa zaidi ya asilimia 43, ukilinganisha na vyandarua vya kawaida. Matumizi ya vyandarua hivyo, yanatarajiwa kusaidia sana udhibiti wa athari zinazotokana na usugu. Aidha, dawa mpya za kutibu malaria na chanjo aina mbili za watoto, tayari zimepitishwa na Shirika la Afya Duniani ili kuanza kutumika. Nchi kadhaa za Afrika, tayari zimeanza kutumia zana hizo mpya za udhibiti wa malaria.

Kuongezeka matumizi ya afua hizi, kutasaidia kufikia lengo la kutokomeza malaria, na kufanikisha hili, tunahitaji nguvu ya pamoja na ushiriki wa wadau mbalimbali. Udhibiti wa malaria ni kichocheo muhimu cha kuonesha utayari wa namna ya kukabiliana na milipuko ya magonjwa, madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa, utoaji huduma za afya ya msingi, na huduma ya afya kwa wote wenye uhitaji. Ni muhimu sana kufanya kazi kwa juhudi ili kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuhamasisha rasilimali kutoka vyanzo vya ndani. Mabaraza ya kutokomeza malaria na magonjwa yasiyopewa kipaumbele ambapo mpaka sasa yamefanikisha kukusanya zaidi ya dola za marekani milioni hamsini (50M).

## Hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji:

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikiwa kupata rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji endelevu wa afua za ugawaji wa vyandarua, ununuzi wa dawa mseto za malaria na vitendanishi kwa kipindi chote cha ruzuku (2024-26). Aidha inaendelea na utaratibu wa kufuatilia taarifa ya makundi ya viuatilifu ambayo yameonesha usugu kwa mbu waenezao malaria tangu mwaka 2015, na kila mwaka imekuwa ikitoa taarifa ya usugu kwa Shirika la Afya Duniani. Kutokana na ufuatiliaji huo, taarifa ya usugu wa makundi ya viuatilifu imesaidia sana kuishauri wizara na kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya vyandarua venye ubora na ufanisi zaidi.

Aidha, Tanzania imeendelea na utaratibu wa kupima na kufuatilia ubora na ufanisi wa dawa za kutibu malaria, tangu mwaka 2018, ili kugundua uwepo wa usugu mapema, na kuripoti matokeo ya ufuatiliaji huo Shirika la Afya Duniani. Mpango Mkakati wa Kudhibiti Malaria, umejumuisha pia afua zinazolenga kuwafikia wakimbizi, na kuonesha namna dhana nzima ya uongozi katika kusimamia udhibiti wa malaria na ushiriki kwenye ***Mpango maalum kwa nchi zilizo na athari ya maambukizi makubwa ya malaria*** – (HBHI), na hatimae kufanikiwa kuanzisha na kuzindua ***Kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na Mimi.***

Sambamba na ajenda ya vipaumbele kama ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wa sasa wa ALMA, Mhe. Umaro Sissoco Embaló, ambae ni Rais wa Jamhuri ya Guinea Bissau, Tanzania imeboresha sana mbinu za uwajibikaji na kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya udhibiti wa malaria, na tayari imeanzisha matumizi ya Kadi Maalum ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaj, ikiwa ni kitovu cha kuchambua na kufanyia kazi takwimu za viashiria toka mikoani, ili kujipanga vizuri zaidi kuelekea kutokomeza malaria nchini. Tanzania tayari imezindua Baraza la Kutokomeza Malaria.

## Matokeo:

Taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2022, inaonesha kuwa idadi ya wagonjwa wa malaria ilikuwa 3,666,741 na idadi ya vifo vilivyotokana na malaria vilikuwa 1,538.

## Changamoto kuu:

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kuna changamoto zilizojitokeza ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi. Changamoto hizo ni pamoja na;

- Kudumisha ajenda muhimu ya utashi wa kisiasa na kutenga fedha kwa ajili ya Zanzibar, hasa ikizingatiwa kuwa maambukizi ya malaria visiwani humo yanaendelea kupungua.

- Kushughulikia upungufu wa rasilimali fedha, ili kuweza kutekeleza kikamilifu na kwa ufanisi Mpango Mkakati wa Malaria nchini.

- Kufuatilia kwa karibu tishio la uwepo wa usugu wa viuatilifu na dawa za kutibu malaria.

## Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyopita:

| Lengo | Vipengele vya Utekelezaji | Muda wa Kukamilisha Utekelezaji | Hatua ya Utekelezaji | Ufafanuzi wa shughuli ukilinganisha na taarifa ya utekelezaji wa robo iliyotangulia. |
|---|---|---|---|---|
| Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali. | Kuziba mapengo muhimu katika ufadhili udhibiti wa Malaria. | Ifikapo robo ya 4, mwaka 2024. | | Tanzania imeweka kipaumbele katika afua za malaria kwa kuzingatia ukubwa na mtawanyo wa hatari ya maambukizi, ili kufikia malengo ya kudhibiti malaria kwa kutumia vyandarua vilivyowekwa viuatilifu katika maeneo yenye maambukizi makubwa na ya kati ya malaria, hasa kwa jamii inayoishi maeneo ya vijijini.<br><br>Mahitaji halisi kwa ajili ya afua ya matibabu ya malaria yanajulikana vyema, ingawa changamoto iliyopo ni upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kushughulikia usugu wa dawa za kutibu malaria.<br><br>Hivi karibuni, Tanzania **ilizindua Baraza la Kutokomeza Malaria** ambalo linashirikiana na Mpango wa Taifa wa kudhibiti malaria, ili kuainisha maeneo ya kipaumbele yenye upungufu, ambayo yanayohitaji fedha za utekelezaji.<br><br>Fedha zipo kupitia ufadhili wa PMI, ili kuendelea kufuatilia ubora na ufanisi wa dawa za kutibu malaria (TES) kwenye maeneo yenye hatari ya maambukizi makubwa na ya kati ya malaria. Mpango wa Taifa wa kudhibiti malaria umeunda kikosi kazi ili kupitia taarifa za ufanisi wa dawa za malaria, ambazo zitasaidia kukabiliana na usugu wa dawa za kutibu malaria kulingana na mazingira ya maeneo husika. |

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetekeleza maazimio kuhusu huduma ya matibabu ya malaria ngazi ya jamii na inaendelea kufuatilia maendeleo kadri hatua hii inavyotekelezwa.

### Hatua Mpya ya Mapendekezo

| Lengo | Vipengele vya Utekelezaji | Muda wa Kukamilisha Utekelezaji |
|---|---|---|
| Lengo | Kuandaa Mpango - Kazi ili kusaidia utekelezaji wa Tamko la Yaoundé | Robo ya 4 2024 |

## Huduma ya Afya ya Uzazi kwa Mama, Mtoto, Mchanga na Vijana.

## Hatua iliyofikiwa.

Tanzania imefanikiwa kufikia kiwango cha juu katika kiashiria cha ugawaji wa vidonge vya *Vitamini A* kwa jamii. Aidha, imeimarisha sana utaratibu wa kusimamia, kufuatilia na uwajibikaji katika utekelezaji huo. Aidha imezindua ***Kadi Maalum ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji*** inayojumuisha viashiria vya huduma ya Afya ya uzazi kwa mama, mtoto mchanga, mtoto na vijana pamoja na kushirikisha wadau katika eneo la lishe.

## Magonjwa yalikuwa hayapewi kipaumbele.

## Hatua iliyofikiwa:

Mafanikio ya kudhibiti magonjwa ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele, yanapimwa kwa kutumia fahirisi ya kielezo kinachozingatia kiwango cha utekelezaji wa tiba-kinga kwa magonjwa ya matende, usubi, kichocho na trakoma.

Mwaka 2022, kiwango cha utekelezaji wa tiba-kinga kilikuwa ni asilimia 38 katika udhibiti wa kichocho, asilimia 78 kwa usubi, asilimia 84 kwa matende na asilimia 86 kwa trakoma. Kwa ujumla kiwango cha utekelezaji kwa magonjwa yasiyopewa kipaumbele kwa Tanzania kwa mwaka 2022 ni alama 68, ikiwa ni ongezeko la alama 5, ukilinganisha na kiwango cha mwaka 2021 ambapo thamani ya kielezo ilikuwa alama 63.

Tanzania imefikia malengo ya Shirika la Afya Duniani katika ugawaji wa dawa-kinga za matende na trakoma. Nchi imeboresha sana mifumo ya ufuatiliaji na uwajibikaji na kufanikisha kuandaa ***Kadi ya Alama ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji wa malaria*** inayojumuisha magonjwa ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele.

Aidha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imesaini Tamko la Kigali.